# *Baba, Saa Imekwisha Kufika*

Asante, Ndugu Joseph. Asante. Twaweza kuomba?

2 Baba yetu, tunakushukuru Wewe, leo hii, kwa ajili ya Bwana Yesu, kwa ajili ya neema Yake kwetu, ya kwamba tulipokuwa tungali wenye dhambi, Kristo alikufa badala yetu ili atuhesabie haki sisi, waovu, na kuturudisha katika ushirika pamoja na Baba, kupitia upatanisho kwa Damu Yake Mwenyewe pale Kalvari, ambapo Yeye aliitoa bure kwa ajili yetu sisi sote. Na, leo, tunafurahia majaliwa haya, kwa sababu Yeye alikuwa tayari.

3 Na sasa, Baba, jalia tuwe tayari kwenda na kushiriki baraka hii kuu pamoja na wengine. Tusaidie kukujua Wewe vyema zaidi kwa kukusanyika alasiri ya leo, kwa kuwa tunaomba hayo, katika Jina la Kristo. Amina.

Ketini.

4 Nina furaha kuona, leo, mchungaji mwenyeji wetu (Ndugu James Jones) kutoka Indianapolis, kule nyuma. Nina furaha sana, na ndugu kutoka Spindale, pia; Ndugu Winston Hare kutoka California. Ninaamini nilipotazama tu, nilimwona Ndugu Sothmann hapa aliyekuwa wa mwisho kutoka—kutoka Canada, ambapo ndio kwanza tuwe na mkutano mkubwa kule juu. Na marafiki wengine wengi wanaoketi humu. Hakika ni majaliwa, leo, kuzungumza na umati kama huo wa watu, ambao ninatazamia kuishi nao Milele, Utukufuni. Nami nina majaliwa leo hii ya kusimama kuzungumza na kushirikiana nanyi kwenye Neno la Mungu. Na hakika ni majaliwa kufanya hivi.

5 Sasa, jana jioni tulikuwa na wakati mzuri katika Bwana, Roho Mtakatifu kweli alimimina baraka Zake juu yetu jana usiku kiajabu sana. Na usiku wa leo tutafanya mstari wa maombi wa mtindo wa kale ambao tulikuwa nao miaka mingi iliyopita. Kwa sababu tutaninii . . . Ni, nilipaswa kuzungumza nanyi muda kidogo alasiri ya leo, kushirikiana nanyi kwenye Neno, halafu, usiku wa leo ninene tena. Na wakati mwingine kwa njia hiyo u—upako wa Roho Mtakatifu kwa ajili ya maono hayo ya Kiungu hauji kama unavyopaswa ikiwa kidogo umefadhaika. Si ninii . . . Simaanishi kufadhaika, ninamaanisha kuwa na shauku kupita kiasi ama kitu kama hicho, haionekani kufanya kazi sawa kabisa. Kwa hiyo Ndugu Joseph, nilimwambia ningependa kuwa na usiku mmoja wa huo kabla ya kuondoka. Naye amekuwa mwema sana kutupa sisi na kupanga hivyo.

6 Na sasa, ninamtarajia Mungu kuwaponya wengi wa wagonjwa na wanaoteseka. Nitawauliza wavulana kama—

kama wataendelea na kusambaza kadi za maombi kwa vyovyote vile, idadi kubwa ya hizo usiku wa leo, ili tuweze kuweka utaratibu katika mstari wa maombi kuwapitisha wagonjwa. Kwa hivyo ikiwa una wapendwa wowote wanaohitaji maombi, nawe unaamini ya kwamba "kuwekewa mikono" ni nguvu za Mungu za kuwaponya wagonjwa siku hizi, mbona, waleteni huku usiku wa leo, maana tunatarajia kuwapitisha wengi wao mstarini.

7 Na sasa, ni muda mfupi sana tulio nao wa kuzungumza, na ninii sana. . .mengi sana ya kuongea. Maadamu tunazungumza juu ya Bwana Yesu, tunayo mengi ya kuzungumzia, jinsi ambavyo kila Neno limevuviwa sana. Nami nitamwomba Mchungaji Joseph kama atajiandaa kunisomea fungu la maneno, ama—ama, kusoma Maandiko, kwa kuwa mimi. . . jambo lingine limekuja niani mwangu sasa hivi, nami nina Agano Jipya pekee, kwa hiyo nataka asome ninii. . .kwa ajili ya msingi, kutoka kwenye Agano la Kale, Mambo ya Nyakati ya Pili 18:22-27. Nitamwomba atusomee hili, nanyi mnaweza kulisoma pamoja naye, mkipenda, kama msingi wa somo langu alasiri ya leo. [Ndugu Joseph Boze anasema, "Mambo ya Nyakati ya Pili?"—Mh.] 18:22 hadi yapata—yapata 27. Bwana na aongeze baraka Zake sasa kwenye kusomwa kwa Neno Lake.

8 Wakati anaponinii. . .mnapolifungua, nitamwomba ndugu huyu hapa kutoka California, je, umesikia lolote kuhusu mkutano tunaouendea, ni wakati gani tutakuwa huko mjini mwako, huko Oakland na kupitia huko? Ndugu walikuwa wanautayarisha siku chache zilizopita, nami. . . [Ndugu mmoja anasema, "Sijasikia lolote bado."—Mh.] Naam, bwana. ["Huenda niliukosa katika safari yangu ya kuja hapa."] Vema, asante, ndugu. Naam, vema. Asante. Nilishangaa tu, itakuwa. . . Nadhani tutaelekea mashariki baada ya Idaho mnamo Novemba na Desemba, na kuja huko Januari au Februari, nafikiri ndivyo, mwishoni mwa Januari, mwanzoni mwa Februari, ama mojawapo, sehemu hii nyingine inapaswa kuwa huku juu mashariki. Au labda, watatoa hiyo kwa Pwani ya Magharibi na kisha waende mashariki. Lakini natumaini kuwaona kule, ndugu, kusikia baadhi ya mafundisho hayo mazuri. Vema, Ndugu Joseph. En-he, 22 hadi 27.

9 [Ndugu Boze anasoma Mambo ya Nyakati ya Pili 18:22-27—Mh.]

> [*Basi sasa, angalia, Bwana ametia pepo wa uongo vinywani mwa manabii wako hawa, naye Bwana amesema mabaya juu yako.*]

> [*Ndipo Zedekia, mwana wa Kenaana, akakaribia, akampiga Mikaya kofi la shavu, akasema, Alitokaje kwangu Roho ya Bwana ili aseme na wewe?*]

[*Mikaya akasema, Angalia, utaona siku ile, utakapoingia katika chumba cha ndani ili ujifiche.*]

[*Ndipo mfalme wa Israeli akasema, Mchukueni Mikaya, mkamrudishe kwa Amoni, liwali wa mji, na kwa Yoashi mwana wa mfalme;*]

[*Mkaseme, Mfalme asema hivi, Mtieni huyu gerezani, mkamlishe chakula cha dhiki, na maji ya shida, hata nitakaporudi kwa amani.*]

[*Naye Mikaya akasema, Ukirudi kabisa kwa amani, basi* BWANA *hakusema kwa mimi. Akasema, Sikieni, enyi watu wote.*]

10 Sasa, katika m—mlango wa 17 wa Yohana Mtakatifu, nasoma kwa ajili ya fungu:

*Maneno hayo aliyasema Yesu, akainua macho yake kuelekea mbinguni, akasema, Baba, saa imekwisha kufika;. . .*

Na aongeze baraka Zake kwenye Neno Lake.

11 Leo, tukifikiria kutumia hili kama jukwaa, kusomwa kwa Neno ambalo. . .kutoka katika Agano la Kale, kwa ajili ya jukwaa la somo katika Agano Jipya, na kuomba kwamba Mungu atatupa muktadha tunapomngojea.

12 Wakati huu katika Agano la Kale ulikuwa wa—wa. . . ulikuwa wakati wa mashaka sana. Sasa, Yehoshafati alikuwa mfalme wa Yuda wakati huo, huku Ahabu akiwa mfalme wa Israeli wakati huo; walikuwa wamegawanyika. Na wakati wowote ambapo, tunapogawanyika, tunaweza kutazamia matatizo. Hatuna budi kuungana, ndipo tutasimama.

13 Na, lakini Yehoshafati alikuwa m—mtu mwenye haki, mtu mwema. Alikuwa amelelewa vizuri na mifano mingi, kama ambayo tumekuwa nayo siku hizi. Alimwona baba yake, Asa, jinsi ambavyo wakati Asa alipomtumikia Bwana, basi Mungu alikuwa pamoja naye; lakini Asa aliposhindwa kumtumikia Bwana na kuwa mkaidi, ndipo Mungu akamwacha.

14 Haidhuru Bwana anatupenda vizuri jinsi gani, na jinsi unavyompenda Bwana, unapoacha kumtumikia na kumwabudu Bwana, basi kumbuka tu, unaweza kutarajia kuibuka kwa matatizo. Kwa sababu Mungu alimwambia Daudi wakati mmoja, "Wewe ni mtu anayeupendeza moyo Wangu Mwenyewe." Ndipo Daudi alipofanya makosa, ilimbidi Daudi kuvuna kile alichopanda. Nasi. . .Yeye kamwe hajatuambia kwamba tuliupendeza moyo Wake Mwenyewe, kwa hiyo hakika itatubidi kuvuna kile tulichopanda.

15 Lakini mnamo wakati huu, Asa alishikwa na ugonjwa miguuni mwake, naye akafa nao, kwa sababu hakumwomba Bwana uponyaji wa Kiungu; alienda kwa madaktari pekee. Asingemwomba Bwana; alikuwa mkaidi sana. Naye alifikia

tu mahali ambapo angeanza kusikiliza maoni ya kisasa wala hakuamini, labda, ama hakuamini kwamba Bwana aliponya, kwa hiyo hakumtaka Bwana shauri lolote juu yake. Aliwazia, "Naam, daktari wangu hawezi kunisaidia; hakuna haja ya kumwomba mtu mwingine yeyote." Kwa hiyo Biblia ilisema alilala. Alipelekwa kwenye makaburi ya baba yake. . .baba zake, na huko akapumzika.

16 Na sasa, Yehoshafati mwanawe, akiinuka kupachukua mahali pake, alikuwa na msingi mzuri wa kutazama, kuona kwamba wakati mtu atatembea kwa ajili ya Mungu na kutembea pamoja na Mungu, Mungu atatembea pamoja na mtu huyo. Lakini wakati mtu yuyo huyo anapompa Mungu kisogo, basi Mungu humwacha tu ajitegemee mwenyewe. Nasi tunagundua ni—ni jambo la kusikitisha sana tunapolazimika kujitegemea wenyewe.

17 Sijaribu kamwe kutumainia hekima yangu mwenyewe, kwa sababu sina yoyote. Ninafurahi sana kwamba sina. Kama ningekuwa nayo, labda ningejaribu kuitegemea. Lakini Bwana aliona tu inafaa kwamba sikuwa nayo, kwa hivyo sina budi kumtumaini Yeye. Na ninaamini lingekuwa ni jambo jema ikiwa sote tungejaribu tu hilo kwa muda kidogo, sivyo? Tusichukue tu mawazo yetu wenyewe kuhusu jambo fulani, bali tutulie kwa uchaji juu ya BWANA ASEMA HIVI. Usijaribu kulihoji, maana huwezi kulihoji. Kama unaweza kulihoji na kuona jinsi hasa litakavyokuwa, lisingekuwa ni tendo la imani tena.

18 Imani ni kile huoni; ni kile unachoamini, ambacho huninii. . .huioni, lakini kuna Kitu ndani yako, kinachoiona. Na huyo ni Mungu aliye ndani, analiona Neno Lake Mwenyewe likidhihirishwa. Lakini usingeweza kulihoji. Ninaninii tu. . . Hakuna njia ya kulifanya. Mungu kamwe hawezi kuhojiwa, kwa sababu Yeye amepita kuhojiwa; Yeye ni Mungu. Nasi tunachukua tu yale aliyosema juu yake na kuyaita kweli.

19 Sasa, katika mkutano huu mkubwa leo, na wakati hili likiendelea, na tukiwa na ushirika huu mkuu, kwa namna fulani niliwazia, labda, kwamba maneno machache tu juu ya jinsi ya kuyawasilisha kwa watu; kwa sababu tukijua kwamba wengi wenu hapa mmeniacha kwa mbali inapofikia ku—kufundisha Maandiko. Nami ni—ninajua kwa hakika, kunao watu wanaoketi hapa ambao, jamani, ambao najisikia duni kusimama hapa karibu nao. Lakini kwa sababu kwamba—kwamba tumehusishwa pamoja, ningependa kutoa maoni yangu ya jinsi lilivyo, na—na onyo langu kwa wale wanaokataa kutembea katika njia ya Mungu ambayo ametuagiza tuiendee.

20 Sasa, kwenye wakati huu Ahabu alikuwa mfalme wa Israeli, naye alizembea sana. Tunao watu kama hao siku hizi, wale kidogo ningewaita mwaminio mkwamia mpakani. Yeye huenda tu kwa njia yoyote u—upepo unayovumia. Ninaamini sisi, siku

hizi, tunaiita "kuhamahama misheni." Na vyovyote tu upepo unavyovuma, wameweka matanga yao waingie humo. Biblia haitaki tuwe hivyo. Yeye anatutaka tuwe imara, tusitikisike, tushikilie sikuzote, tuyaelekeze matanga yetu moja kwa moja Kalvari. Ikiwa upepo unavuma kinyume, kuna njia ya kulidhibiti tanga hilo, au, meli, na kuufanya upepo huo, ingawa unaukabili uso wako moja kwa moja, unaweza kuabiri moja kwa moja kwenye huo upepo; ni jinsi unavyoweka tanga lako. Jambo ndilo hilo.

21 Nasi tunaweka meli yetu tuliyokodisha kuelekea Kalvari, na haidhuru upepo unavuma kwa njia gani, bado tunaiangalia Kalvari, iwe ni kinyume, ama iwe chochote kile, tungali tumeelekea Kalvari. Huyo ndiye mwaminio wa kweli. Na ndipo hatutupwi huku na huku na kila upepo wa mafundisho, na *hili* linaingia, na *lile* linaingia, na *hili* linatukia; tunayo njia moja tu thabiti: hiyo ni moja kwa moja hadi Kalvari.

22 Nafikiri hivyo ndivyo Mungu alivyomaanisha aliponena kupitia Yuda, na . . . kule, na akasema, "Wingu lisilo na mvua, nyota zipoteazo . . . " wakitangatanga tu. Hiyo ni—hiyo si sawa; hatupaswi kufanya hivyo. Tunapaswa tu . . . Wakati Mkristo anapozaliwa mara ya kwanza katika Ufalme wa Mungu, mapenzi yake, maisha yake, kila kitu kinawekwa moja kwa moja juu ya Kristo. Ikiwa yeye ni mwerevu kidogo, usipokuwa mwangalifu, atayaweka yote juu ya elimu kisha awe baridi kabisa, wa kirasmi, na asiyejali, na kila kitu, theolojia kidogo, ama tafsiri kuu ya maneno ya Kiyunani.

23 Nilikutana na mtu hapa muda fulani uliopita, naye akasema, "Billy, ndiyo kwanza nijifunze neno fulani la Kiyunani. Nimelifuatilia miaka mitano, nikijaribu kujua maana halisi ya neno hili la Kiyunani." Kasema, "Loo, nilipolipata, ni baraka."

Nikasema, "Ati umekuwa ukilifuatilia Neno moja la Kiyunani miaka mitano?"

"Naam."

24 Nikasema, "Katika miaka hiyo mitano, kwa neema ya Mungu, nimewavuta watu nusu milioni kwa Kristo bila kujua neno lolote la Kiyunani." Kwa hiyo hiyo ni, si yale unayojua, ni Yule unayemjua: Kumjua Yeye ni Uzima. Nasi tunatumia muda mwingi sana kwenye mambo hayo ambayo ni ya kipumbavu. Ninii tu, simaanishi upumbavu, ambayo hayatufai kitu. Ukiisha kulijua, linakufaa nini? Hakuna. Kwa hiyo afadhali umjue Yeye.

25 Na basi kama atakuwa, mtu huyu anayemzingatia Kristo, ikiwa ana wasiwasi kidogo au wa mhemko, usipomtazama mtu huyo, atapeperuka kuelekea upande *huu*, aingie kwenye ulokole. Naye atakuwa wa kawaida . . . kila upande upepo unaovuma, huyu hapa anaenda. Kila mahali mchachariko unapotokea, mbona, ataufuata.

26 Lakini hutaki hiyo. Mmoja ni kinyume tu kama huo mwingine ulivyo. Lakini tunataka kuweka matumaini yetu, Kristo na hapo peke yake. Mtazame Mwana-kondoo wa Mungu. Tazama upate kuishi.

27 Sasa, na kwa hiyo Yehoshafati alikuwa ameona, wakati baba yake alipomtegemea Mungu, ya kwamba Mungu alimbariki. Naye alikuwa ameona kwamba Ahabu alimwacha Mungu, kwa sababu mke wake hakutaka aende kanisani Jumatano usiku, na kadhalika, mnajua. Kwa hiyo wakagundua kwamba amekuwa vuguvugu, asiye na msimamo, anayepelekwa huku na huku.

28 Mnajua, ninaamini kama sikumwamini Kristo, ningekuwa kinyume Naye kabisa. Pia ninaamini kama ningejielezea, na moyoni mwangu nilikuwa kinyume Naye wala sikumwamini, kama ningejifanya adui Wake, angeniheshimu zaidi, kuliko vile angeniheshimu kama nisingekuwa na msimamo, ninatupwa huku na huku. Hiyo ni kweli.

29 Ninaamini ya kwamba hata katika maisha ya mwanadamu. . . Unamchukua mwanamke, msichana. . . Sasa, sisi ni shule tu, darasa. Msichana, huenda asiwe mrembo, lakini kama yeye ni mama halisi, na anashikilia mahali pake kama mama mwenye heshima, mnajua ataheshimiwa zaidi kuliko mwanamke mrembo asiyepashika mahali pake. Mnaona? Hiyo ni kweli. Maana ni. . . Mwanamume yeyote ambaye ana wakia ndogo ya uanamume juu yake, ataheshimu ukweli huo na uaminifu.

30 Na halafu, kama tukiwa Mkristo, lazima tuweke uaminifu wote, na staha, na heshima kwa Bwana Yesu Kristo. Halafu basi, kama sivyo tulivyo, wala hatuamini, usiwe tu bila msimamo kulihusu, acha tu ulimwengu ujue mahali unaposimama; hiyo ndiyo njia bora kabisa. Basi itakuwa ni siku kuu wakati kanisa litakapofikia mahali hapo, washiriki wake, hasa. Ambapo kama. . . Itakuwa ama ni upande wa Kristo au dhidi ya Kristo. Ndipo ulimwengu mzima utajua jinsi unavyosimama.

31 Sipendi mtu yeyote kunipapasapapasa begani na kusema, "Sasa, Ndugu Branham, ninakupenda kweli." Huku akijua ya kwamba najua vinginevyo, (Mnaona?), ye—yeye anajua kuwa najua vinginevyo. Maana roho yake haitoshei vizuri, wala ha—haipo mle kabisa. Na kwa hiyo, mimi—mimi, basi, ninapoteza heshima kwa mtu huyo.

32 Na—napenda kumwona mwanaume ikiwa alisema, "Sasa, tazama, si—sikubaliani na wewe, juu ya hilo. Mimi. . . " Vema, basi yeye ni mwaminifu juu yake. Lakini Ahabu hakuwa mtu wa aina hiyo; alikuwa mtu ambaye alitaka ku—kumtumikia Bwana wakati mmoja, naye mke wake alitaka kufanya jambo tofauti; ndipo akageuka upande huo, na kuagiza manabii wauawe, na kadhalika, mmoja wa hao wasio na msimamo, juu-chini, wanaoingia na kutoka; wala Mungu hawezi kamwe kufanya

lolote na mtu kama huyo. Asingeweza katika siku hiyo, wala siku yoyote, asingeweza kumtumia mtu kama huyo.

33 Kwa hiyo tunaona: Lakini Yehoshafati alikuwa ameona matokeo ya maisha ya namna hiyo; alikuwa ameona matokeo kutoka kwa baba yake alipomtumikia Bwana, kisha wakati hakumtumikia Bwana. Kwa hiyo yote hayo kwa pamoja, na kuyazingatia, Yehoshafati alikuwa amekusudia moyoni mwake kumtumikia Bwana na kushikamana na mambo ambayo baba yake, Daudi, alifanya hapo mwanzo. Ninapenda hiyo: "Hapo mwanzo . . . " Biblia ilisema.

34 Kwa maneno mengine, alirudi kwenye alama ya kale ya mpakani kisha wakatengeneza safu. Ingekuwa vyema kwa Pentekoste kurudi kwenye alama ya kale ya mpakani. Ingekuwa vyema kwetu sote kurudi kwenye alama za kale za mpakani na kuzitengeneza safu. Ingekuwaje leo katika ninii . . . Ninazungumza, nadhani, zaidi sana na Wapentekoste hapa alasiri ya leo. Je, ingekuwaje kama, kwa kweli, kanisa lingerudi kwenye alama ya kale ya mpakani? Nena kuhusu kusafisha, kweli kungekuwako na kumoja kwenye kanisa la Kipentekoste; hakika kungekuwako. Sasa, ni wangapi wanaojua hiyo ni kweli? Mbona, hakika, naam. Hakika kungekuwako na . . . hakika, ma—matengenezo yakiendelea. Loo, jinsi watu wangekuwa wanatenda tofauti, wanavalia tofauti, wanazungumza tofauti, nalo lingekuwa—lingekuwa tu ni kanisa tofauti kabisa, kama tungerudi kwenye alama ya kale ya mpakani tulikoanzia.

35 Sasa, kwa hiyo basi Mungu akambariki. Mungu atambariki mtu yeyote ambaye atarudi kwenye alama ya kale ya mpakani ya Biblia na kuanzia kwenye Biblia, si kulingana na theolojia, bali kutokana na, au, theolojia fulani ya kujibunia, bali kutoka kwenye theolojia ya kweli ya Biblia, na kuanzia kwenye alama ya kale ya mpakani na kwenda mbele, Mungu atakwenda pamoja nawe.

36 Kwa hiyo Mungu akaanza kumbariki Yehoshafati, na muda si muda mwajua, akaanza kumfanikisha. Naye akajenga zile ngome zote, ili kwamba wasiotahiriwa na wale . . . wasiweze kuingia. Na hiyo ndiyo makanisa yanayohitaji siku hizi, ni ngome ya mafundisho ya kale ya kimitume, kusudi huu uvuguvugu, urasmi, wa kuingia-na-kutoka, juu-chini, usiingie kanisani mwetu.

37 Ningesema nini? Hiyo ni kweli, hata hivyo. Hiyo ni kweli. Tumeruhusu mambo mengi mno kuingia ndani, ndugu, mambo mengi sana, ambapo tuliacha alama ya kale ya mpakani tangu mwanzo, kunyemelea ndani; kamwe hatukulilinda kanisa. Na sasa tuna kila kitu ndani yake. Hiyo ni kweli. "Itikadi" zote na "hitikadi" na—na chochote kile kanisani, kwa maana hatukulikinga kwa Neno.

38 Nilikuwa nikizungumza leo kwenye chakula cha mchana na Ndugu duPlessis na Ndugu Joseph, nasi tulikuwa tukizungumza kuhusu misheni za ugenini na uamsho wa dunia nzima, kwamba, safari ya misheni ya ulimwenguni kote ambayo ninajiandaa kufanya kote ulimwenguni, katika kila jiji siku chache usiku, kila jiji kuu ulimwenguni. Kisha nikiwazia juu ya ufuatiliaji nikasema, "Ni kama . . . "

Wakasema, "Ikiwa huna ufuatiliaji, basi unapoteza kile u—ulichokiendea."

39 Kama nilikuwa na ri—risasi mkononi mwangu. Niwaambie jinsi risasi hiyo ilivyosifika, jinsi kasimwelekeo ya risasi hii itakavyopenya kwa umbali fulani, na kwamba ina mwe—mwe—mwendo gani inapotoka, itasafiri kwa mwendo wa futi elfu tano kwa sekunde, juu ya bunduki ya mtindo wa kale ambayo labda itaenda mwendo wa, loo, futi elfu moja kwa sekunde. Sasa, hiyo risasi ni sawa, kama nikikiweka hicho . . . ki—kibweta cha risasi mkononi mwako, lakini unaweza kufanya nini nacho? Huna bunduki ya kuitumia.

40 Kwa hiyo, haya basi. Hatuna budi kuwa na ufuatiliaji; inabidi tuwe na ngome; hatuna budi kuliweka kanisa katika utaratibu, likienda taratibu, kundi kubwa la kwenda mbele. Tunapoteza tu wakati mpaka kanisa litakapoingia katika hali ya namna hiyo. Tutawapata wachache *hapa*, hiyo ni kweli; lakini si kama vile tungekuwa kama sote tungekuwa kundi moja kubwa lisilogawanyika la watu, kundi moja kubwa.

41 Adui . . . Katika jeshi ikiwa sehemu yao . . . ikiwa Wakentaki wanawashambulia Wahoosia, nao Wahoosia wanawashambulia Wakentaki, Wailinoi wakipigana na Wamisiouri, katika vita, mbona, yale majeshi yatasimama tu kando na kusema, "Acheni wauane wenyewe." Lakini wakati wote wameungana, hapo ndipo adui anapoinua masikio yake juu na kutoroka. Na wakati jeshi lote kuu la Mungu litakapoungana pamoja chini ya bendera moja, uongozi wa Roho Mtakatifu, na kusonga mbele kama Kanisa kuu la Mungu aliye hai, ndipo adui atakimbia. Yeye hana budi kukimbia.

42 Nasi tunaona katika Biblia mfano wetu. Kwa hiyo ukiona, baada ya Mungu kumbariki mtu huyu mkuu, Yehoshafati, kumfanikisha na kila kitu kikaanza kwenda sawa, siku moja aliwazia angemtembelea jirani yake, Ahabu. Naye alipokuwa akishuka kwenda kumtembelea Ahabu, aliwazia, "Vema, nitakuwa na ushirika huko chini." Sasa, hapo ndipo alipofanya kosa, papo hapo, maana mafuta na maji havitachanganyikana. Hiyo ni kweli. Wala mwaminio na asiyeamini hawatachanganyikana pamoja; huna budi kuwa upande mmoja ama mwingine. Inabidi uchukue msimamo, na uendelee kusimama.

43 Kwa hiyo aliposhuka kwenda kumwona Ahabu, loo, ni mapokezi ya jinsi gani aliyopata. Loo jamani, Ahabu akachinja maksai, na kondoo, na kadhalika, na wana-kondoo, na kufanya karamu kubwa na. . . Sasa, hivyo ndivyo tu adui anavyoingia. Hivyo ndivyo tu alivyofanya kwenu ninyi akina dada. Alipoanza, mwanamke fulani aliingia, nalo kanisa likaanza kumpigapiga mgongoni, naye a—alikuwa mwanamke aliyekata nywele, na kujipodoa, na mambo kama hayo. Muda si muda mwajua, ilianza kuingia polepole, na sasa kanisa zima limechanganyikiwa katika hilo. Amina. Hiyo ni kweli. Sasa, ninyi. . . Msiache liwaudhi. Lakini tunahitaji upasuaji. Hiyo ni kweli.

44 Basi wakati mwanamume alipofikia mahali ambapo yeye hakuwa mwanamume, mumewe, na kumwacha afanye jambo hilo, hilo lilionyesha udhaifu wake. Hiyo ni kweli. Anapaswa kuwa ndiye kiongozi wa nyumba.

45 Kwa hiyo, lakini siku hizi taifa zima liko katika mwelekeo huo. Na Marekani si Marekani tena kweli; si taifa la Kikristo tena; ni taifa la mwanamke. Maskini Yezebeli anashuka mtaani akiwa amejipaka rangi kwelikweli, na, ndugu, wanaume watampigia magoti. Hiyo ni kweli. Najua hilo kidogo linaudhi, lakini huo ndio ukweli. Tunahitaji upasuaji.

46 Sasa, hayo yako ulimwenguni, pamoja na Hollywood. Hayo hayako tu ulimwenguni na Hollywood, hayo yako katika kanisa la Kipentekoste. Hatujalindwa dhidi ya mambo hayo. Naye mchungaji alikuwa dhaifu vya kutosha kuwaruhusu waendelee nayo. Kama ungepiga makelele dhidi ya jambo hilo, kanisa zima katika jeshi moja kubwa lililoungana, basi lingekoma muda mrefu uliopita. Lakini loo, tumefikia sasa ambapo si tofauti; wanafanya lolote wanalotaka kufanya: ukombozi wa wanawake, wanavaa nguo hizi za kale zinazoonekana mbaya, zisizo na adabu, kisha wanaenda mtaani.

47 Na hebu niseme jambo fulani papa hapa, mama yangu. Natumaini nyote mnanipenda, wala siko hapa kuwakosoa; Niko hapa tu kujua kwamba huko ng'ambo, kwenye Siku ya Hukumu, itanibidi kuwajibika, wakati nikijua mambo haya wala nisiwaambie; halafu basi nikiwaonya, basi damu imetoka mikononi mwangu.

48 Je, mlijua Yesu Kristo alisema, "Kila mtu amtazamaye mwanamke kwa kumtamani, amekwisha kuzini naye moyoni mwake." Je, kuna mtu yeyote anayejua hilo? Bi-. . . Na ukijivalisha kwa kuvutia kizinifu, haidhuru unawazia ni ya kiasi jinsi gani, na kwenda nje mtaani, naye maskini mwenye dhambi fulani akuangalie kwa kukutamani, kwenye Kizimba cha Hukumu utakuwa na hatia ya kufanya uzinzi na mtu huyo atakapowajibika kwake. Ni kwa nini? Ilikuwa ni wewe, wewe ndiye uliyefanya hilo; ulijianika hivyo, kwa hiyo wewe ndiye mwenye hatia. Nawe, haijalishi umeishi bikira na safi jinsi gani,

utakuwa na hatia mbele za Mungu ya kufanya uzinzi na mwenye dhambi, kama tu kwamba ulitenda tendo hilo. Yesu alisema hivyo. Hayo si mambo ya juujuu, ndugu; huo ndio ukweli. Ni seng'enge. Lakini ni vile Neno la Mungu linavyosema, linakata, na lina makali kuliko upanga ukatao kuwili.

49 Sijui kama mchungaji wako atathamini hilo au la. Lakini ninakwambia, dada yangu, kwenye Kizimba cha Hukumu itanibidi kuwajibika kwake, na nisiposema mambo haya... Sijali ni watu wangapi wanasema "ukombozi wa wanawake," hilo ni fundisho la ibilisi. Wala haliko katika Biblia hii. Hiyo ni kweli.

50 Mnaona kile kilichotukia huko Rumi; mnaona kilichotukia huko Uyunani; mnaona kilichotokea huko nyuma katika makoloni ya kale ya Kirumi zamani, kwa kanisa la Kikristo walipoanza kutenda kama ulimwengu. Mnaijua hiyo historia, ama, mchungaji wenu anapaswa kuwafundisha. Nanyi mnaona katika kila zama kile kinachotukia kwa kundi hilo. Nanyi mnaona mahali lilipo hasa sasa hivi katika kanisa la Kipentekoste. Kwa hiyo ni wakati wa kuchora mstari, na kufanya ngome, na kuhubiri ukweli. Mna mifano, sawa na vile Yehoshafati alivyokuwa na mifano. Kwa hiyo hebu tuchore mstari wetu, tujinyooshe, na tutembee kama wanaume na wanawake wanavyopaswa kufanya, na kujiwasilisha wenyewe.

51 Sasa, mwanamume, bila shaka katika mavazi yake, yeye si...ni ninii...yeye si mtakatifu, au, si mtu aliye na mwili kama wa mwanamke; tunatambua hilo. Sasa, ni wanawake. Na wanawake ni wa ajabu sana.

52 Nimeitwa mchukia wanawake. Mtu yeyote anayesema hivyo...usifanye...kuna—kuna kasoro. Siwachukii. Lakini na—nawapenda, nami ninataka wawe binti za Mungu, na kutenda kama binti za Mungu, sawa tu na wanaume. Hatuna budi kufanya hivyo.

53 Kwa hivyo tunaona mambo hayo kama mfano, na wakati ninyi wanakamati hapa, wakati mkutano wenu unapoendelea, ndugu, mna shida gani? Mnasoma Biblia ile ile; mnajua Biblia inafundisha mambo hayo. Kwa hivyo hebu tulishughulikie. Hebu tuwe upande wa Mungu au tuwe dhidi ya Mungu. Ni lini Mungu alijibu kwa zaidi? Wakati tulitenda kama Wakristo au sasa? Mbona, huduma ya John Wesley ingeinuka na kukilaani kizazi hiki cha Kipentekoste, huko nyuma katika wakati wa utakatifu wa kale.

54 Sasa, mnajua hiyo ni kweli. John Wesley aliheshimika zaidi katika mafundisho yake, na katika lile kanisa la mtindo wa kale zamani za kale, kuliko sisi Wapentekoste tulivyowahi kuwa. Hiyo ni kweli. Angalia walichofanya; walifanya mambo ambayo sisi hatujui lolote kuyahusu. Vema, Mungu aliwaheshimu na

kuwabariki, kwa sababu walitembea kwa unyofu mbele za Mungu. Hiyo ni kweli. Na tunajua kuwa huo ni mfano.

55 Sasa, lakini aliposhuka na kufanya ushirika na Ahabu, ndipo akapata matatizo. Sasa, Ahabu. . .Nanyi mnapouchukua ulimwengu ambao unajaribu kufanya ushirika pamoja nanyi, kumbukeni tu, kuna mtego mkubwa mahali fulani.

56 Unapomchukua maskini mvulana huyo anayevuta sigara, ambaye anataka kukupeleka nje usiku, ewe msichana, ewe msichana wa Kipentekoste, maskini huyo mlevi, na nywele zake zimechanwa vilivyo, laini sana kiasi cha kufungua kinywa chake. Hebu nikwambie kitu fulani sasa; kuna mtego unaowekwa. Ati naye anasema, "Nitakuoa, mpenzi, ikiwa. . .Kisha ni—nitajiunga na kanisa lenu." Anakudanganya. Ikiwa anakupenda na kumpenda Bwana, atafanya hivyo wakati huo; sio lazima akuchukue. Hiyo ni kweli. Nanyi wanaume, ninyi wavulana wadogo pamoja na baadhi ya Mayezebeli hawa wadogo waliojipaka rangi, vivyo hivyo. Hampaswi kufanya hivyo.

57 Aibu kwa wachungaji wanaoshindwa kusema hivyo kanisani mwao. Sisi ni watu walioitwa, waliotengwa, tofauti, waliotakaswa kwa Bwana katika Israeli. Naam, bwana, tunajua alama za mpakani; zimeandikwa papa *hapa* chini, mtazamo wake waziwazi. Lakini tunayumbishwa tu. Huyu anaingia, akasema, "Yote *haya*, *yale*, na *haya* yote, *yale*." Tunashindwa tu, tunaanguka nayo moja kwa moja. Hakika. Biblia ilisema ibilisi atakuwa akifanya hivyo katika siku za mwisho. Na hivyo ndivyo hasa anavyofanya.

58 Sasa, ndipo akamfanyia karamu kubwa na kumwalika. Sasa, alikuwa na kusudi fulani la kufanya hivyo, alisema. . . maana alijua alikuwa mtu mwenye nguvu sana, basi akasema, "Sasa, hebu tuyaunganishe makundi yetu pamoja, na tuungane katika jeshi moja kubwa mno, kisha tutapanda kwenda Ramoth-gileadi. Ndipo—ndipo basi tukienda kule, tutamshinda adui, kwa maana eneo *fulani* hili ni letu hata hivyo. Ramoth-gileadi ni mali yetu. Na kwa kweli ni milki yetu, kwa hiyo basi utusaidie kukwea huko tukachukue mali iliyo yetu." Unaona, mwenye tamaa.

59 Na hapo ndipo Yehoshafati alifanya kosa lake. Ndipo akiwa mtu wa kiroho hata hivyo, alisema, "Naam, nitakwenda pamoja nawe, lakini kwanza, hebu tumtake Bwana shauri." Hilo hapo jambo zuri: ombea kila jambo.

60 Na kisha akasema, "Vema, tutafanya hivyo tu. Sasa, nina seminari hapa chini; nina baadhi ya manabii bora zaidi waliopo. Loo, wamesoma kwelikweli. Hao ndio watu werevu zaidi walioko nchini, maana nimelizingatia. Nimeshughulika nao. Ninaisaidia seminari. Nami ninao walio bora zaidi, kwa hiyo nitawaita wateule waje."

61 Kwa hiyo akaenda na kuwachukua wasomi wote wazuri na kuwaleta kule. Ndipo wote wakakusanyika pamoja: mia nne wao. Naye akasema, "Hivi sisi...?" Naweza kumwona huyo mfalme. Na kila mtu, wakienenda tu moja kwa moja jinsi... chochote asemacho mfalme; chochote askofu asemacho, wote wanatenda, mnajua. Mwangalizi mkuu, mwajua, anachosema, wote wanafanya. Mnaona? Mkono kotini nwake, mwajua, na kusema, "Sasa, mabwana, je, nipande kwenda Ramoth-gileadi au niache?"

62 Mmoja akasema, "Mnajua huyo ni nani, sivyo? Mnajua ambapo riziki yetu inatoka; tutatengwa; hatutakuwa na *hili*, na hatutakuwa na kitu cha kutusaidia. Um-hum, sasa afadhali mwe waangalifu."

"Unasemaje kuhusu hilo, mchungaji?"

"Vema, nawaambia; naona ni afadhali."

"Naam, nafikiri hivyo pia. Vipi kuhusu msimamizi, anasemaje?"

63 "Loo, analipitisha neno hilo moja kwa moja; afadhali sote tuseme mema juu ya mfalme." Loo, jamani. Afadhali tuseme, "Loo, hili ndilo dhehebu kuu sana lililopo, wala hakuna mfano wake; hakuna kinachoweza kufanya hivyo ila hili. Sisi pekee ndio tulio na kauli juu yake."

Basi wote wakatoka nje na moyo mmoja, wakasema, "Loo, Bwana asema, 'Kwea; Yeye yuko pamoja nawe.'"

Ahabu akasema, "Unaona, hakika, tutakwea."

64 Lakini mnajua, kulikuwa na kitu fulani kuhusu mtu wa kiroho, wakati ni...haijalishi ni wangapi wanasema "ndiyo," kama ni kinyume na Neno, mtu huyo haliamini. Yehoshafati akasema, "Vema, kwani una wangapi huko nje?"

65 Kasema, "Mia nne. Na wote ni wanafunzi wa seminari; ni watu mashuhuri; na kwa moyo mmoja wanatupa lililo kweli; loo, hatuna budi kushinda tu."

Naye akasema, "Lakini—lakini—lakini—lakini—lakini huna mmoja zaidi?"

66 "Vema, unahitaji mmoja zaidi wa nini? Hawa hapa mia nne, walio bora sana; mmoja zaidi angeleta tofauti gani, ikiwa una mia nne wanaosema, 'Ndiyo'? Vema, kwa nini kuomba mmoja zaidi?"

Akasema, "Lakini wajua, hivi huna mmoja zaidi?"

67 Akasema, "Naam, nina maskini mtakatifu anayejifingirisha hapa chini, bali yeye..." Vema, yeye ni mtakatifu anayejifingirisha; alikuwa mtu aliyetengwa, mnajua, akasema. Akasema, "Nina mmoja hapa chini, lakini namchukia." Loo, naam, hakika, hapana budi, alimwudhi wakati wote. Yeye kidogo ni kisirani; akamparuza kidogo. Akasema,

"Nitakwambia kabla hajaja, ninamchukia," akasema, "kwa sababu sikuzote husema mabaya juu yangu." Hakika, angefanya nini tena? Neno lilisema mabaya juu yake.

68 Kwa hiyo ningewezaje kunyamaza kuhusu wanawake Wakristo kujipaka rangi? Ningewezaje kunyamaza juu ya udhaifu wa kanisa la Kikristo wakati Neno linaupinga? Hakika, naam; Neno linaupinga. Sijali mchungaji anasema nini; Neno linasema hivyo; hebu tudumu kwenye Neno. Mia nne walikuwa wakitoa kauli moja, kwamba ilikuwa sawa kuondoka kwenda vitani. "Naam, hiyo ni kweli; loo, haitadhuru chochote; msimwamini, a—ana akili finyu."

69 Lakini Mikaya alikuwa na ukweli. Huo ndio tunaotaka, ni ukweli. Haidhuru unaumiza wapi, unakotahiri, au unamkatilia nani mbali, tunataka ukweli. "Mtaifahamu kweli, nayo hiyo kweli itawaweka huru." Amina. Loo, hakika.

Loo, akasema, "Wao . . . Angalia walio nao; wanalo kundi lile la watakatifu wanaojifingirisha huko juu sasa. Msikilizeni sasa."

70 Lakini nataka mtambue, kabla hajafika pale, walituma kamati kumlaki, ikasema, "Sasa tazama, wavulana wote wa seminari ya theolojia wako kule juu, na kila mmoja amemwambia mfalme ilikuwa ni sawa kwake kwenda kufanya anachotaka kufanya. Sasa, Mikaya, usiseme chochote kinyume na wanachosema. Sasa, atataka kuunganisha pamoja sasa. Unataka kusema sawasawa na analosema."

Kama ingalikuwa ni kulingana na Neno, ingalikuwa ni sawa; lakini ilikuwa kinyume na Neno. Hiyo ni kweli.

71 Kama vile mhudumu mmoja hapa si muda mrefu uliopita alivyokuwa akisema; alikuwa anaenda . . . mwinjilisti, akienda kanisani kufanya m—mkutano. Na ninatumai hamtalichukulia hili kama mzaha, kwa sababu si mahali pa utani; nilihakikishiwa kwamba ni kweli. Na ilidhaniwa kuwa katika kanisa zuri la kimadhehebu.

Basi halmashauri ya mashemasi ilikutana naye chini mahali fulani kwenye gari-moshi, nao wakapanda, na kusema, "Je, wewe ndiye yule mwinjilisti?"

Akasema, "Naam." Alikuwa akisoma Biblia yake, akiandika muhtasari kidogo alipokuwa akisoma na kuomba.

Akasema, "Sasa, tulitumwa, kama kamati kutoka kanisani, kukwambia sasa, mambo machache kuhusu kanisa letu."

72 Akasema, "Sawa, ningependa kuyasikia kabla sijafika huko, nipate kujua zaidi jinsi ya kulikaribia hilo kanisa pamoja na hao watu." Akasema, "Nataka kuwa baraka kwenu niwapo huko."

73 Kasema, "Vema, hivyo ndivyo tunavyokutaka uwe. Sasa, tunakwambia tu, mwinjilisti, kwamba, usiseme chochote kuhusu mbio za farasi," kasema, "kwa sababu mchungaji ana uwanja wa mashindano ya mbio za farasi," kisha akasema, "naye sikuzote

huweka dau kwenye hizo mbio. Nasi tusingekuruhusu udhuru hisia za mchungaji wetu, hapana."

74 Kisha akasema sasa, "Kwa kawaida wainjilisti huwa ni vimondo vya moto," kisha kasema, "tuna mawazo bora kuliko hayo kwako, kwa hiyo, au, usiseme chochote. . . Kawaida wao hushambulia michezo hii hapa ya Karata kanisani." Kasema, "Sasa, Shirika la Misaada la Wanawake sikuzote huwa na mchezo wa Karata kila Jumatano usiku, baada ya mkutano wa maombi, katika chumba cha chini. Kwa hiyo kuwa na hakika, usiseme chochote kuhusu hilo." Ndipo akaendelea na orodha nzima ya mambo, ambayo asingeweza kugusia, asingeweza kuyazungumzia.

Huyo mwinjilisti akasema, "Basi nitazungumza juu ya nini?"

Naye akasema, "Unaweza kuzungumza juu ya Wayahudi, kwa sababu tuna mmoja tu wa hao kanisani."

75 Sasa, kuna uinjilisti kama huo siku hizi katika Pentekoste. Wanahofu kusema ukweli. Kweli. Sijali ikiwa inamwudhi mchungaji au inamwudhi nani; ni Neno la Milele la Mungu. Nasi tunawajibika kwake, kuhubiri kwake. Hatuna budi kusema ukweli; sijali jinsi unavyoudhi.

76 Lakini unajua, walizungumza na mtu asiyefaa walipozungumza na Mikaya namna hiyo. Loo, hapana, hakuwa mmoja wa hawa waridhiaji aliyetega mabawa yake aone kama atapata sadaka nono au la. Loo, hapana, hapana, hapana. Alikuwa mtu wa Mungu.

77 Mbona, ningeweza kuwazia, Maandiko hayasemi hivyo, lakini huenda labda wangesema, "Sasa, kama utasema jambo lile lile, yale manabii hawa wasemayo, kutoka katika seminari, unajua nini? Wanaweza kukupa digrii kutoka chuo hicho. Unajua, wanaweza kabisa, baada ya kitambo kidogo, ukiisha kujifunza kuongea sarufi bora zaidi, unajua nini? Kwa kweli wanaweza kukufanya kuwa mmoja wao, endapo utasema jambo lile lile wanalosema." Loo, naam, watafanya hivyo hata wa leo, pia. Hakika, watafanya.

78 Lakini huyu mtakatifu anayejifingirisha alisema nini? Alisema, "Nitasema tu kile ambacho Mungu wangu ataweka kinywani mwangu kusema." Amina. Huyo hapo mtu mnayepaswa kuwa naye.

79 Si ajabu Roho Mtakatifu mle ndani ya moyo wa Yehoshafati, alisema, "Bado kuna mmoja zaidi; atawaambia ukweli; atawaambia ukweli. Mmoja tu zaidi, lakini kweli atakuwa mkweli kwako."

80 Kwa hiyo basi, maskini Mikaya akaja huko, akiisha kuomba na kuona ono. Naye Yehoshafati akaketi, amezungukwa na wahubiri wake wote mia nne, Dk., Ph.D., na hao wengine wote, mwajua, karibu na pale, na msimamizi mkuu, na a—

askofu, naye . . . wote hao, mnajua, walikuwa wamepazunguka pale. Loo, ushirika mkuu, wakila mnofu wa nyama ya kondoo na kadhalika, wakiwa na wakati mzuri sana. Nao wote walikuwa wamevaa nadhifu kabisa, ukosi wao umepinduliwa, na magauni yao marefu yakining'inia, mwajua, na "baba mtakatifu" limeandikwa juu yao, na kila kitu kama wafanyavyo, mnajua, wamevalia nadhifu kwelikweli.

81 Lakini mnajua, hilo halikumpendeza huyo mtu wa Mungu moyoni mwake. Alidhani kuna kitu tofauti na hicho. Nami pia; kweli nadhani hivyo. Inanikumbusha juu ya Sauli akijaribu kumvika Daudi fulana yake ya kikanisa; kamwe halikufaa kitu kwa mtu wa Mungu; hivyo tu. Kamwe halimwenei vizuri, kasema, "Ondoa kitu hiki hapa, sijawahi kukithibitisha."

82 Sasa, hilo ndilo tunalohitaji siku hizi, ni kuvua baadhi ya fulana zetu za kikanisa na kuvaa haki ya Yesu Kristo, tujaribu kuachana na kunena maneno makuu mno ambapo wote hao, kusanyiko halijui tunazungumzia nini kwa vyovyote vile. Hiyo ni kweli. Maskini mahubiri ya mtindo wa kale wa mashambani ndiyo yatakayowaokoa. Ni ukweli. Haidhuru ni thabiti jinsi gani, ni—ni Neno kwa vyovyote vile; wanalielewa hivyo. Sisi si matajiri na wa kisasa katika mambo haya yote makubwa mno; sisi ni wa mtindo wa kale, au tunapaswa kuwa hivyo. Sasa, si lazima tujifunze jinsi ya kutumia sarufi kuu na kufanya maneno haya yote makuu na kadhalika, yanene tu waziwazi.

Ndipo ikawaje? Ni wakati wa jinsi gani. Jambo linalofuata tunaloona, ya kwamba hawa wasomi maarufu wamesimama pande zote . . .

83 Na hebu nizungumze hili kwa dakika moja tu. Je, unajua tabaka hutoka wapi? Tabaka ni la ibilisi. Sasa, hiyo ni BWANA ASEMA HIVI kwa Biblia. Tabaka na fahari vilitoka kwa ibilisi. Hapo mwanzo kabisa Kaini na Habili walipopanda kuja kuabudu, Kaini alikuja mbele za Bwana katika tabaka. Habili alikuja katika haki kwa ufunuo.

84 Sasa, angalieni, Kaini alipokuja, alileta matunda ya kondeni, kila kitu kiotacho, maua na kila kitu, naye akayapamba madhabahu yake, kisha akamwabudu Mungu; picha ya kweli ya mfuasi wa kanisa la kimwili siku hizi, na mchungaji mwenye nia ya kimwili ambaye anataka kanisa lililowekwa juu zaidi ya hayo mengine yote mjini, na—na viti vyao vyote vimepambwa, na kinanda cha bomba cha dola milioni moja. Mungu hajali [Ndugu Branham anadata vidole vyake—Mh.] *hivyo* kwa hilo. Kweli, halina uhusiano . . . Unajenga maeneo hayo yote makubwa namna hiyo na kuwasumbua watu wako mpaka angalau wanakuwa maskini hohehahe na chochote kile pamoja na vitu vyako vyote vya kuweka kanisani, na maelfu ya makafiri wakifa kwenye huduma za kimisheni pasipo kumjua Kristo wakati mmoja. Kweli, ni aibu kwa Ukristo. Naam.

85 Loo, laiti ungaliweza kuona wakati mmoja, ungejua nilichokuwa nikizungumzia. Kujenga kanisa la dola milioni moja, na theluthi mbili za ulimwengu hawakuwahi kusikia habari za Yesu Kristo; ni jambo la kusikitisha jinsi gani.

86 Sasa, mwangalie. Wakati huo ilikuwa ni tabaka, naye Kaini akaja amepakwa mafuta na Shetani na kufanya jambo kubwa sana la kitabaka. Lakini sasa, Habili, alipokuja, kamwe hakuja kitabaka, bali alikuja katika ufunuo. Biblia ilisema katika Waebrania 3 kwamba, "Habili kwa imani alimtolea Mungu dhabihu iliyo bora kuliko ya Kaini." Na njia pekee aliyofanya hivyo ilikuwa kwa imani na imani katika nini? Neno la Mungu, maana hilo ndilo jambo pekee unaloweza kuwa na imani nalo. Mungu alikuwa amemfunulia ya kwamba ilikuwa ni ile damu. Naye Kaini alikuwa na dhabihu ya kupendeza, ila haikufunikwa kwa damu. Naye Habili hakuwa na sadaka ya kupendeza, bali ilikuwa imefunikwa katika damu, na iliambatana na Neno. Naye Mungu akaitambua, kwa maana lilikuwa ni Neno Lake.

87 Na leo hii, Mungu haangalii kanisa kubwa, jinsi ya kujenga . . . mjenzi wake mkubwa, jinsi kwa—kwaya inavyoweza kuimba vizuri, ama yote *haya*, *mengineyo*, ama ni watu wa tabaka gani, kama wamevalia vizuri, ama hawajavaa vizuri, kanisani mwenu. Haangalii mambo kama hayo, hapana, si kwa maili milioni moja, hayaangalii hayo.

88 Anatarajia mtu aje kupitia njia ya Damu, ufunuo. Naye Habili, kwa imani, alisikia Neno la Mungu, na akaliamini Neno la Mungu; na kwa imani katika Neno la Mungu, Mungu akampokea. Hiyo ndiyo njia pekee ambayo Mungu atampokea mtu yeyote, ni kwa kuliamini Neno la Mungu kwa ufunuo kwamba Mungu atalitimiza Neno Lake.

89 Mungu alisema Roho Mtakatifu anafaa siku hizi; hilo latosha kwangu. Ikiwa Mungu aliweka nguvu kanisani kuwaponya wagonjwa na kutoa pepo; na manabii na kadhalika, akawaweka kanisani, na akaahidi, kwamba wangekuwako hata mwisho wa dunia; hilo linaniridhisha. Sijali yale mwanatheolojia yeyote, au ni kiasi gani wanaweza kufanya kama mdudu kwenye limau, kukimbia *hapa*, kufinya *hapa*, kufinya *pale*; haileti tofauti hata kidogo. Mungu alisema hivyo, na hilo latosha. Hebu tudumu na Mungu; tuliamini Neno Lake.

90 Sasa, Mungu alimwambia Kaini, akasema, "Kama ukitenda vyema, (Mnaona?), lakini usipofanya hivyo, dhambi inakuotea mlangoni." Hakika. Kaini alikuwa mfano wa mwaminio wa kimwili siku hizi, anayeshuka na kuwazia, "Nitajiunga . . . Angalia, unajua kanisa kubwa lililoko Chicago, ni *Nanii* na Dak. *Nanii*. Nitaenda nikajiunge nalo huko."

91 Kisha unaenda unasoma kwenye Biblia na kugundua kwamba hakuna hata moja ya mambo ambayo Yesu alisema yataendelea kanisani, "Ishara hizi zitafuatana na hao,

waaminio," hazifuatani nao. Yesu alisema zitafuatana na hao waaminio, si labda huenda zitafuatana nao, huenda ikawa zitafuatana nao, zitafuatana nao kwa muda fulani wa wakati. Alisema, "Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio." Na iliahidiwa hata mwisho wa ulimwengu. Nataka ukurasa na Maandiko ambapo Yeye alisema aliwanyang'anya. Basi angelipinga Neno Lake Mwenyewe. Mnaona jinsi mngeingia kwenye mchafuko mkubwa? "Ishara hizi zitafuatana na hao." Hiyo ilikuwa ni alama, kumbukumbu, alama ya waaminio wa kweli, ya kwamba Yeye alikuwa katikati yao. Maana anajionyesha Mwenyewe na kujidhihirisha Mwenyewe kwa ishara hizi. Amina.

92 Sasa, kuwazia, kanisa lililojengwa juu ya hilo, kuuachilia ulimwengu upenye ndani? Mbona, hakika itaiamsha hasira ya mtumishi wa kweli wa Mungu. Hakika, ni makosa; hebu tuondoeni kitu hicho humo. Tuachane na uvuguvugu huu wa kale, nusunusu, kukariri sala ndogo asubuhi, sala ndogo usiku, kisha kwenda kulala, na kuamka kesho yake asubuhi. Si ajabu tunakuwa wa kilimwengu. Si ajabu ulimwengu umepenya ukaingia kanisani, kwa sababu hatudumu katika maombi. Hakuna kuugua tena; hakuna kukaa tena mbele za Mungu; hakuna tena kuchimba, kusafisha. Tunahitaji uamsho wa mtindo wa kale. Tunajivuta tu, "Sisi ni Assemblies. Sisi ni Wapentekoste. Sisi ni wa Umoja. Sisi ni wa Utatu. Sisi ni *hiki*, *kile*, ama *kinginecho*. Hatuna uhusiano wowote na kundi hilo lingine."

93 Hapo ndipo Roho Mtakatifu anapokuacha, papo hapo. Unapotia jambo hilo niani mwako, ndugu, afadhali tu urudi madhabahuni, kwa sababu hapo ndipo mahali pako. Hiyo ni kweli. Amina. Hivyo ndivyo ulimwengu unavyopenya ndani. Hebu tusahau hilo. Hebu tuweke upendo wetu juu ya Kristo na kumtazama Kristo na Yeye pekee, amina, na tuwe na ushirika sisi kwa sisi, huku Damu ya Yesu Kristo ikitusafisha na dhambi zote. Kama angekuja kumtia alama, leo hii, kila mmoja wetu asiye na kosa, angemtia nani alama?

94 Ikiwa unafikiri huyo mtu mwingine yuko makosani, kumbuka, neema ya Mungu ni halisi kwake tu kama ilivyo kwako. Ningechukia Yeye kunitia alama leo hii, kama nilikuwa bila hatia au la. Sina imani na hilo; ninatumaini katika neema ya Bwana Yesu Kristo kunipitisha. Ninasimama katika neema Yake pekee. Sina cha mikononi ninacholeta. Sijafanya chochote; sijasema kitu kisicho na thamani yoyote.

95 Hakuna jambo nililofanya, Bwana, nakutegemea tu Wewe kabisa, Wewe tu, na Wewe peke yako. Hakika, Bwana, na kama ninakupenda kwa moyo wa kweli, bila shaka nitakupenda, na kutembea, na kujaribu niwezavyo nisifanye lolote la kukuudhi Wewe. Na kama nitakufanyia jambo lolote baya, nitalitubia upesi mara nikilifanya.

96 Ninampenda mke wangu, kama ningemfanyia jambo lolote baya, ningelitubia mara moja, kama nililifanya bila kujua. Au ningetubu, na kumwambia nilijutia kulifanya, hakika kama vile ningefanya kwa Bwana wangu. Wala kamwe nisingefanya chochote cha kumdhuru maskini huyo mke. Na wala singefanya hivyo kumwudhi Mungu mara milioni zaidi ya mke wangu. Ikiwa unampenda, utamheshimu, utatembea sawasawa.

97 Hapo, angalieni, lakini kilichotupoteza, ni juu ya theolojia yetu. Loo, jamani. "Unajua, Dk. *Nanii*, yeye ni mtu maarufu. Loo, mnajua anazungumza kwa lugha mbili au tatu mbalimbali? Anafanya yote *haya*, *yale*, na *mengineyo*. Unajua nini? Yeye alichunga kanisa kuu la *Ninii* wakati mmoja." Sasa, hilo si ni jambo? "Loo, unapaswa kusikia jinsi asemavyo, 'Ah-miina.' Ni nzuri mno."

98 Nilisoma makala gazetini hivi majuzi, marefu *hivi*, ambapo yalisema kwamba askofu *fulani* wa kanisa *fulani,* aliomba maombi mazuri sana kwa dhehebu *fulani* ambayo yamepata kuombwa. Hilo ndilo aliloomba, hilo dhehebu, si Kristo. Hiyo ni kweli; ilichukua kama nusu ya ukurasa wa gazeti kuandika maombi yake. Aliliomba hilo dhehebu, maombi mazuri. Loo.

99 Na hilo linalijilia la Pentekoste pia. "Loo, naam, tunaparembesha mahali hapo sana, tunafanya mambo yavutie sana, na kuonekana ya kupendeza sana." Hakika, tunakuwa kama hao wengine. Ni wakati wa kujitikisa; kutoka humo. Hiyo ni kweli.

100 Vipi kuhusu ile Damu? Usiwe kama sadaka ya Kaini. Weka Damu juu yako; sijali jinsi ilivyo na sura mbaya, na ni mbichi, na lugha mbaya, na vyovyote vile ilivyo; weka Damu. Hiyo ndiyo tunayohitaji. Dumu chini ya Damu.

101 Tunaona, huyu mwenye umaarufu. Naam, Mungu alimpa nafasi. Akasema, "Sasa, kama utafanya vyema, itakuwa sawa; utakubalika. Lakini usipofanya vyema, basi dhambi iko mlangoni. Sasa, umeona ya kwamba nimeukubali m—mpango huu hapa, wala sijaikubali yako. Lakini sasa, kama utafanya vyema, utakuja huku na kushiriki hapa. 'Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio.' Na kama ukiona nimelikubali fundisho hilo, Biblia Yangu, nimelishika Neno Langu, nimelithibitisha miongoni mwa watu, sasa kama utafanya vyema, njoo pamoja nao. Hebu tufanye ushirika sisi kwa sisi."

102 Lakini Kaini alifanya nini? Kama tu wanavyofanya siku hizi; alitafuta namna ya kumweka nje ya utaratibu. Hiyo ni kweli. Ndugu, siku moja, usijali, kama wewe ni Mkristo wa kweli kabisa, ngozi yako itawekwa mnada. Hiyo ni. . .Hilo lisikutie hofu. Na sasa hivi unachukiwa miongoni mwa watu wote kwa ajili ya Jina Lake, umedharauliwa na kukataliwa. Unaona?

Naye akasema, "Sasa, kama ukitenda vyema. . ." Lakini hakutenda vyema; lakini akamwua ndugu yake.

103 Sikuzote ni wenye umaarufu; lakini haidhuru wahubiri hawa wote ni maarufu jinsi gani, na mbele ya wafalme hawa wawili, hata hivyo, Mikaya akasema, "Niliona la-. . .katika maono, Mungu ameketi juu ya kiti Chake cha enzi, na jeshi la Mbinguni limesimama mkono Wake wa kuume na wa kushoto. Nao wakasema, 'Tunaweza kumtuma nani ashuke akamdanganye Ahabu, kumpeleka huko nje kutimiza Neno la Mungu?'"

104 Ukitaka kuona maono, ukitaka kuwa sahihi, dumu katika Neno. Mungu hutenda kazi moja kwa moja katika Neno; huo ndio mpango. Mnaona? Sasa, Mikaya . . . Sikilizeni, hii hapa siri: Mikaya alikuwa anakaa sawasawa na kile nabii alichosema, nabii Eliya, kwa sababu Ahabu alikuwa amefanya uovu, alisema, "Mbwa watailamba damu yako . . . " Na jinsi . . . " . . . juu ya kifo cha Nabothi mwenye haki."

105 Na jinsi ambavyo Neno la Mungu kupitia kwa nabii huyo, ambalo lilikuwa ni Neno la Mungu, linavyomjia nabii, nao walidumu moja kwa moja nalo. Wala Mikaya asingeweza kwenda kulia wala kushoto kutoka kwalo, kwa maana lilikuwa tayari limethibitishwa ni Neno la Mungu. Kweli. Neno la Mungu lilikuwa pamoja na manabii katika siku hizo. Yeye alikuwa na torati, bali aliweka Neno Lake kwa manabii. Naye Mikaya, akiwa nabii, nabii wa kweli . . .

106 Sasa, angalieni, hebu niwaonyeshe jambo fulani. Loo, naliona. Angalieni hapa; hili ni jipya. Kulikuwako na wanafunzi mia nne wa seminari waliodai kulijua Neno wala hawakuwa wanaliheshimu. Walijaribu kulikwepa kwa sababu ya fahari. Walijaribu kulikwepa kwa sababu ilikuwa ni mfalme, kumpigapiga mtu mgongoni.

107 Lakini maskini huyu "mtakatifu anayejifingirisha," kama nilivyomwita muda mfupi uliopita, hakujali kupiga-piga-mgongoni kuliendelea kiasi gani, alidumu na Neno la Mungu. Naye asingeweza kutabiri chochote, ama kuhubiri wakati huo, ila yale Neno liliyosema. Amina. Utukufu! Dumu pamoja na Neno, hilo hapo, ndugu. Mungu atalitetea Neno hilo kila wakati. Hakujali seminari zilifundisha nini; hakujali yeyote kati ya hao wengine alikuwa ni nini; alijua Neno la Mungu lilitangaza laana juu ya Ahabu, wala hakuna kitu kingine kingeweza kupachukua mahali pake.

108 Kwa hiyo basi, akiwa pamoja na Neno na kuambatana na Neno, Roho Mtakatifu akaambatana naye, au, akaambatana pamoja na Roho Mtakatifu na kuona ono. Vema, utukufu! Ninajisikia vizuri sana, kubarikiwa kweli. Shika Neno, dumu na Neno. Na kama kamwe, ono la kweli likiwahi kutokea, litakuja kwa Neno. Amina. Sijawahi kuwazia hilo hapo awali, hilo ni jipya. Asante Bwana. Kaa na Neno, ndugu.

109 Eliya, ama, Mikaya alikuwa pamoja na Neno, kwa maana Neno lilikuwa limetangaza laana juu ya kitu hicho. Basi Mikaya

angewezaje kusema lingine lolote ila kukaa na Neno? Kwa hiyo kwa kukaa pamoja na Neno, Mungu alimwonyesha mwendeleo wa Neno. Haleluya! Haya basi. Natumaini wewe. . .linazama ndani yako kama linavyozama kwangu. Lakini, hilo hapo. Mungu ataonyesha mwendeleo wa Neno. Kasema, "Hakika, endelea mbele ikiwa unataka. Ni sawa, ondoka ukafanye kile wahubiri wanachokwambia ufanye, lakini niliona Israeli wametawanyika kama kondoo wasio na mchungaji." Kasema, "Nilimwona Mungu Mbinguni; nikaona kiti cha enzi, na jeshi la Mbinguni wamesimama mkono wa kuume na wa kushoto. Kasema, 'Tunaweza kumtuma nani ashuke akamdanganye Ahabu? Tunaweza kumtuma nani ili amlete huku kuutimiza unabii wa Eliya?'"

110 Mnaona, Mikaya alikuwa moja kwa moja kwenye Neno hilo. Neno hilo ilibidi litimizwe. Ndipo pepo mwongo akajitokeza, akatokea kuzimu, akaja pale na kusema, "Ninaweza kukufanyia jambo fulani." Kasema, "Unajua nini? Ninaweza kuingia katika seminari hiyo kwa urahisi, kwa sababu hawana, hawafanyi mikutano mingi ya maombi, hawaugui. Hakuna kitu mahali pale, hakuna Damu, kwa hiyo ninaweza tu kutembea wakati wowote ninapotaka. Um-hum, um-hum. Ninaweza kumiliki kitu hicho, dhehebu hilo lote. Naweza kukichukua kitu hicho chote; hata hawaamini katika Damu. Kwa hiyo ni—ninaweza kuchukua kitu hicho chote."

Mungu akasema, "Hiyo ni kweli, unaweza kufanya hivyo."

111 Kasema, "Nitashuka kule na kuingia ndani ya hao jamaa na kuwafanya watoe unabii wa uongo, hao wahubiri wote. Kila mmoja wao, theolojia yao yote kuu, nitayapofusha tu macho yao kutoka kwa Neno. Hayo ndiyo yote ninayopaswa kufanya ni kuliweka Neno hilo ili wasiweze kuliona."

Mnajua, Mungu hufanya hivyo mara nyingi sana. Kasema, "Wana macho wala hawawezi kuona; masikio wala hawawezi kusikia." Je, hiyo ni kweli? Hakika.

112 Kasema, "Nitayapofusha macho yao, wala hawawezi kuliona. Kwa hiyo nitashuka tu na kuwafanya wavuviwe, nao watatabiri uongo. Ndipo utampandisha huko juu."

113 Na kwa hiyo mmoja wa wahubiri hawa, loo, si—sifa zake kuu zilininii sana (Ningesema nini?), zilidhalilishwa sana mbele ya watu, hata akakaribia na kumpiga kofi usoni. Akasema, "Roho wa Mungu alipitia njia gani kutoka kwangu?"

114 Sasa, aliwazia alikuwa na Roho wa Mungu. Lakini ilikuwa ni roho wa uongo, kwa maana ilikuwa kinyume na Neno. Sasa, kama watu wakisema, "Ishara na maajabu hayafuati," ni roho wa uongo; ni kinyume cha Neno.

115 Kama, "Biblia inasema," watu wakikwambia, "Roho Mtakatifu siku hizi si kama alivyokuwa katika siku zile," ni roho wa uongo aliye ndani ya manabii wa uongo. Wanakwambia

uongo. Kama roho akipata . . . anasema tu, “Ukombozi wote wa wanawake, na kufanya mambo haya mengine yote, na kutoka nje, kutenda kama walimwengu.” Ni roho wa uongo. Haliambatani na Neno, dumu katika Neno. Kweli. Dumu papo hapo.

116 Sasa, nanyi mnajua vile hiyo hadithi ilivyoishia. Ilikuwa ni nini? Miaka ilikuwa imepita. Lakini wakati ulikuwa umekwisha kufika kwa Neno hilo kutimizwa. Wakati msimu unapozunguka, msijali, mazao yatakuwapo. Ni kweli.

117 Na ndugu, kama kumewahi kuwa na wakati . . . Kwa dakika chache zijazo sasa, nataka kuzungumza nanyi, kwa moyo wako. Kama kuliwahi kuwa na wakati, ambapo wakati umefika kwa Neno kutimizwa, ni sasa. Hii ndiyo siku. Mbegu zimepandwa; ni wakati wa kuchukua jembe na kuja huku nje, na kwenda kufyeka baadhi ya magugu haya na kadhalika tuliyoachilia yakue: tukapanda michongoma; na magugu yanayovunda; na chochote kile kilichokua miongoni mwa watu; wenye kushuku; wasioamini; vuguvugu; chochote kile. Wakati umefika kwetu kuchukua jembe na kuyang’oa. Na hakuna kitu bora zaidi kuliko Upanga wa Mungu wenye makali kuwili wa kuyakatia.

Wakati ulikuwa umefika katika ulimwengu uliotangulia gharika kwa Mungu kuonyesha Neno Lake lililofanyika kweli kwa watu wa kabla ya ile gharika. Naye akamheshimu Nuhu.

118 Wakati ulikuwa umefika katika Babeli, ambao wangemcheka Mungu kwa dharau. Waliwadhihaki wa—wana wa Kiebrania. Waliwacheka, wakawaambia walikuwa “maskini wasiofahamu” na kila kitu. “Wanapaswa kuwa wa kisasa.” Lakini walikaa imara. Mungu anaheshimu huko kukaa imara. Nao walikuwa wamewacheka, wakawatupa gerezani, wakawafanyia kila kitu. Lakini hatimaye, wakati ulifika kwa Mungu kunena. Ndipo akaonyesha nguvu Zake. Aliweza kuwakomboa kutoka katika tanuru ya moto. Alionyesha nguvu Zake wakati ulipofika.

119 Danieli alipotupwa katika tundu la simba, wakati ulikuwa umewadia kwa Mungu kutoka na kunena. Naye akafunga kinywa cha simba kwa kumtuma Malaika katika hilo tundu pamoja na Danieli.

120 Yesu, kabla tu ya Kalvari . . . Wakati ulikuwa umewadia ambapo ilibidi tangazo litiwe saini. Ilifikia wakati ambapo jamii ya Adamu ilikuwa mwishoni mwa safari; ilibidi jambo fulani kutendeka. Ulikuwa ni kwenye wakati huo ambapo Zakaria, akisimama Hekaluni, alimwona Malaika wa Mungu, ambaye alimwonya na kumwambia yale yatakayotukia. Wakati ulikuwa umekaribia. Naye alikuwa . . . alitilia shaka Neno la Malaika naye akafanywa bubu.

121 Wakati ulifika ambapo Mariamu alikuwa anatoka kisimani, siku hiyo, akiwa na mtungi wa maji kichwani mwake. Wakati

ulikuwa umefika wa kutembelewa na Mwokozi, naye... kwamba bikira angechukua mimba na kumzaa Mwana. Wakati ulikuwepo, bila kujali yale ambayo ulimwengu hata haukuamini, yote yalikuwa kinyume na mafundisho yao. Lakini wakati ukaja, na huku wakati umewadia, "Litatukia." Amina. Malaika Gabrieli alikutana na huyo bikira na kumwambia angetiwa uvuli na Roho Mtakatifu naye angemzaa Mwana, naye angekuwa ni Mwana wa Mungu. Halijawahi kutokea katika ulimwengu wote, lakini wakati ulikuwa umewadia.

122 Wakati kila mwanamke wa Kiyahudi alikuwa amengoja na kuutazamia wakati wa jambo hili, akitumaini ingekuwa ni yeye. Lakini wakati ulifika ambapo Mungu alifanya chaguo Lake. Mungu huchagua.

123 Wakati ulifika ambapo Yohana Mbatizaji alizaliwa kama mtangulizi wa kutimiza Neno la Mungu. Maana alikuwa ni sauti ya mtu aliaye nyikani: katika Isaya 40, kwamba kungekuwako na mtu, miaka mia kadhaa kabla hajaja. Wakati ulifika wa Yohana kuzaliwa. Na wakati ulipofika, Yohana alijitokeza jukwaani. Amina.

124 Wakati ulikuwa umefika baada ya kifo cha Yesu, baada ya Kalvari, wakati ulifika, pale, ambapo hana budi kufa kwa ajili ya dhambi za ulimwengu. Naye alikufa kulingana tu na Maandiko. Maana kila mtu aliamini jambo hilo, akajiweka sawa na Neno, nao wakati ukafika ambapo halina budi kutimizwa.

125 Naye akafa kati ya wahalifu wawili. Walipita, wakiivunja miguu yao kwa nyundo. Ndipo yule Mrumi akainua ile nyundo ya kupondaponda apate kuuvunja mguu Wake, lakini wakati ulifika ambapo Biblia haina budi kutimizwa, iliposema, "Hakutakuwako na mfupa utakaovunjwa katika mwili Wake"; naye akatulia. Ilikuwa ni nini? Malaika wa Mungu aliuzuia mkono wake. Wakati ulikuwa umefika kwa Maandiko kutimia.

126 Wakamlaza kaburini. Wakatia muhuri juu ya kaburi. Wakaweka kundi la askari, karne, watu mia moja, wenye silaha, pande zote huko kuhakikisha kwamba hakuna jambo lingetukia. Kwa siku tatu alilala pale, kupitia Ijumaa, Jumamosi, na Jumapili. Lakini Jumapili asubuhi, ile Pasaka ya kwanza, haijalishi ni majeshi mangapi yalikuwa pale, jinsi yalivyokuwa yamepazingira vizuri, wakati ulikuwa umefika wa Neno la Mungu kutimia. "Sitamwacha Mtakatifu Wangu aone uharibifu. Wala sitaiacha nafsi Yake katika kuzimu." Wakati ulikuwa umewadia. Sijali kinachotukia, litatukia kwa vyovyote vile. Wakati ulikuwa umewadia. Ndipo Malaika akaja kutoka Mbinguni, nao hao watu wakaanguka kama wafu, ndipo kaburi likafunguka, naye Kristo akatoka akiwa mshindi juu ya mauti, kuzimu, na kaburi. Wakati ulikuwa umewadia. Amina.

127 Baada ya hayo aliwaagiza wanafunzi Wake kwenda ulimwenguni kote, na kuihubiri Injili kwa kila kiumbe.

Akasema, “Kabla hamjaenda, sijali jinsi mlivyoelimishwa vizuri. Sijali ni kiasi gani mumetembea na Mimi. Kabla ya kufanyika shahidi Wangu, hamna budi kungoja kule mpaka mvikwe uweza utokao Juu.” Ilikuwa ni kitu gani? Alikuwa sawa na Neno.

Yoeli akasema, “Itakuwa katika siku za mwisho, nitaimwaga Roho Yangu juu ya wote wenye mwili; wana wenu na binti zenu watatabiri.”

128 Yesu, kabla ya hapo, alisema, “Injili hii ingehubiriwa katika miisho yote ya ulimwengu kwa ushuhuda Wangu, na haina budi kuanzia Yerusalemu.” Luka 24:49.

129 Angalia, ndipo wakapanda chumbani. Mmoja wao angesema, “Naam, tunapaswa kungoja hapa kwa muda gani?”

Mwingine anasema, “Naamini nitatoka nje.”

Naweza kumsikia akisema, “Kamwe hakusema tungoje muda gani, alisema, ‘Ngojeni mpaka mvikwe uweza.’”

“Tutangoja hata lini?”

“Hilo silo swali; hilo silo agizo, ni kungoja hata mtakapovikwa.”

“Je, niombe kwa muda gani? Je, ningoje siku ngapi zaidi? Je, uamsho unapaswa kuanza sasa?”

130 Ndugu, ngoja mpaka Mungu atakapoumwaga uweza Wake. Si mpaka tutakapomchagua askofu mpya, si mpaka tutakapomweka mchungaji mpya, bali ngoja mpaka Roho Mtakatifu aje kutoka Mbinguni, kama upepo wa nguvu ukienda kasi. Sio kungoja mpaka tutakapochagua ni nani atakayekuwa askofu wa kundi hili. Sio kungoja tuone ni nani atakayekuwa mwangalizi wa kikundi hiki. Ati kungoja mpaka mumejipanga wenyewe: la, bwana. Sio kungoja mpaka mumemweka mzee mpya wa wilaya: la, bwana. Sio kungoja hadi uwe na fedha za kutosha kujenga kanisa jipya: la, bwana. Lakini ngoja mpaka uvikwe na uweza utokao Juu. Amina.

131 Ndipo basi, wakati hiyo hesabu kamili ya Kipentekoste ilipotimizwa, siku hamsini, wakati ulikuwa umefika. Haleluya! Wakati ulikuwa umefika wa kutimizwa kwa unabii wa Yoeli. Wakati ulikuwa umefika wa Yesu kumwaga Roho Wake. Wakati ulikuwa umefika wa kutimizwa kwa Neno.

132 Na kulikuwako na mtu aliyejiweka sawa na Neno apate kulitimiza. Utukufu! Ndugu! Na kwa ghafla, kwa wale waliojiweka sawa na Neno, wakiingojea ile Ahadi, “Kukaja sauti kutoka Mbinguni kama uvumi wa upepo wa nguvu ukienda kasi, ukaijaza nyumba yote waliyokuwa wameketi.”

133 Isaya alisema, “Amri juu ya amri; na kanuni juu ya kanuni; huku kidogo, na huku kidogo. Shikilia yaliyo mema. Kwa maana kwa midomo yenye kigugumizi na kwa lugha nyingine nitasema

na watu hawa. Na huku ndiko kuburudisha." Amina. Hii ndiyo raha itakayotoka katika Uwepo wa Bwana.

134 Haijalishi kama hawajawahi kuzungumza tangu Babeli. Lakini ilikuwa, wakati ulikuwa umefika wa Mungu kuyaunganisha mataifa pamoja, nao watu kwa moyo mmoja kwa nia moja, iwe ni lugha gani au chochote kile. Alizungumza katika kila lahaja chini ya mbingu, kundi moja la watu, wote Wagalilaya. Wakati ulikuwa umefika. Amina.

135 Ndugu, wakati umefika. Tuko katika siku za mwisho. Tuko katika enzi ya atomiki. Wakati umefika ambapo wana silaha inayoweza kuitikisa dunia kutoka kwenye mzingo wake, katika muda wa dakika tano, hadi kwenye jua, na kusababisha maangamizi kamili. Hawangeweza kufanya hivyo hapo awali. Lakini wakati umefika. Amina.

136 Wakati umefika ambapo kuna ukengeufu. Biblia ilisema, "Isipokuwa ule ukengeufu uje, yule mtu wa kuasi hatajidhihirisha." Kanisa la Kipentekoste linaishi katika wakati wa ukengeufu. Wakati umefika.

137 Wakati umefika kwa zile ishara kufuatana na waaminio. Tuko kwenye wakati wa mwisho. Tuko kwenye mvua ya vuli. Tuko kwenye wakati ambapo watu watakuwa wakaidi, wenye kujivuna, wapendao anasa kuliko kumpenda Mungu, wasiotaka kufanya suluhu, wasingiziaji, wasiojizuia, na wenye kuwadharau walio wema, wakaidi, na wenye kujivuna. Wakati umefika ambapo wanafundisha mafundisho ya mashetani, wakiyapotosha mafundisho ya Biblia wakayafanya nadharia na theolojia wapate kuyavutia makundi ya watu wawafuate.

138 Ni, wakati umefika ambapo Mungu atalikusanya Kanisa Lake pamoja hivi karibuni chini ya bendera moja kubwa sana, Bwana Yesu Kristo, na kumwaga nguvu Zake miongoni mwao. Ndipo ishara kuu na maajabu yatatokea; wakati umefika.

139 Wakati umefika kwa kanisa la Kipentekoste kuchukua msimamo wake. Wakati umefika wa kulitahiri kanisa na kukomesha upumbavu huu. Wakati umefika wa kurudi kwenye alama ya kale ya mpakani. Wakati umefika wa kule kumwagwa. Wakati umefika wa kuwakusanya watu. Wakati umefika wa Yesu kuja. Wakati utawadia hivi karibuni wa kutoa zawadi.

140 Ndugu, kuwa mwangalifu taji yako isije ikawekwa juu ya kichwa cha mtu mwingine. Wakati umefika. Tuko kwenye wakati wa mwisho. Kama tutawahi kufanya jambo lolote, ndugu, tutalifanya sasa. Wakati umekaribia. Wakati umefika ambapo Mungu analitikisa kila dhehebu chini ya jua.

141 Nilikuwa nikisoma makala ambapo mwanatheolojia mkuu katika kanisa la Kibaptisti alikuja kwenye mojawapo ya ile mikutano, naye akaona kazi ya Roho Mtakatifu. Ilikuwa kwenye *Sauti ya Uponyaji*. Ndugu Boze, atalichapisha tena.

142 Ambapo alisema, “Mwandishi wa Kibaptisti anakutana na nabii wa Kipentekoste.” Naye akavitupa vitabu vyake vyote. Akaitupilia mbali theolojia yake yote, akapiga magoti, na kusema, “Mungu, kama unaweza kufanya hivyo kwa mtu huyo, nifanyie na mimi.” Ndipo taya zake zikafungwa kwa utukufu naye akanena kwa lugha tatu mbalimbali, ndipo akaenda jukwaani akiwaombea wagonjwa naye Mungu akitenda ishara na maajabu. Amina. Utukufu!

143 Wakati umefika ambapo vile vito. . .Wakati umefika kwa watafuta madini kuanza kuchimba. Vito hivyo vinatoka kwenye kila dhehebu, viking’arishwa, na kupewa karama, na kuwekwa katika utaratibu. Haleluya! Wakati umewadia.

144 Wakati umewadia sasa hivi. Ubatizo wa Roho Mtakatifu unapitia mjini tena. Ni wakati wa wenye dhambi kutubu. Ni wakati wa waliorudi nyuma kujiweka sawa na Mungu. Ni wakati wa kufanya usafi kanisani. Ni wakati wa ishara ambazo Mungu alionyesha. Kila mtu aliingojea ishara yao. Zile ishara za Marko 16 zinatimizwa, bila shaka zinatimizwa.

145 Daudi aliingojea ishara. Alisikia; alingojea. Alingojea kuanza. Ndipo mara akasikia vichaka vya miforsadi vikichacharisha. Alijua Mungu alikuwa akimtangulia. Ndugu, wakati umefika ambapo vichaka vya miforsadi vya Kipentekoste vinatikiswa tena kwa kumwagwa kwa Roho Mtakatifu kama alivyoshuka kwenye Siku ya Pentekoste, ule upepo wa nguvu ukienda kasi uliotoka Mbinguni. Wakati umefika, kama watawahi kutenda. Wakati umefika. [Dada mmoja ananena kwa lugha, ndugu mmoja anafasiri—Mh.] Amina. Amina. Amina. Amina. “Iwe hivyo,” asema Bwana. Amina.

146 Sasa, unaposikia Neno, unapomsikia Roho, lugha, tafsiri, zikiambatana na Neno, ni wangapi kati yenu kwa uchaji moyoni mwako utasema, “Ninajua nimekuwa makosani, na tangu, kwa neema ya Mungu, tangu leo hii na kuendelea, ninachukua msimamo kuwa sawa na Kristo”? Je, utasimama kwa miguu yako? Utainuka kwa miguu yako? Kwa hili, kusema, “Sasa ninachukua msimamo wangu kwa ajili ya Yesu, bila kujali. Sasa nachukua msimamo wangu, kwa uchaji.”

Matumaini yangu hayajajengwa juu ya kitu chochote pungufu
Ila Damu ya Yesu na haki;
Wakati yote yanayoizunguka roho yangu yakitoweka,
Basi Yeye ndiye tumaini langu na nanga yangu.

Juu ya Kristo, Mwamba wenye imara, nasimama;
Sakafu zingine zote ni mchanga udidimiao,
Sakafu zingine zote ni mchanga udidimiao.

[Ndugu mmoja anatoa himizo—Mh.] Amina. Ati nini? Tokeni kati yao; mkatengwe nao, endeleeni kujiweka sawa na Neno. Mungu yu pamoja nasi. Mungu anaonyesha mkono Wake katika rehema.

147 Marafiki, nafikiri tunachohitaji kufanya, ni kuvunjika kwa mtindo wa kale mbele za Mungu, kwa uchaji, na kusema, “Mungu, natubu uovu wangu wote; na sasa nisamehe na unisaidie kuwa Mkristo halisi.”

148 Hebu tusiwe—tusiwe na njia nyingine yoyote, lakini moyo uliovunjika wa uovu wetu, wakati Mungu akiwa miongoni mwetu labda kwa mara ya mwisho kwa muda mrefu, ikiwa Yeye yuko katikati yetu sasa kutupa wakati huu wa toba, hebu na tutubu kwa mioyo yetu yote, na kumpa Mungu utukufu, na tuchukue msimamo mpya leo na kumtumikia na tutoke nje. Enyi wanawake, jitakaseni. Enyi wanaume, iweni Wakristo. Enyi wahubiri, nendeni kwenye mimbara yenu mkihubiri. Mungu yu pamoja nasi.

149 Ikiwa kuliwahi kuwa na wakati . . . Nilipokuwa Uswidi, ama, Ufini, walikuwa wakivuta mkokoteni na kulima mashamba wapande mbegu. Kama hawakufanya hivyo, hivi karibuni theluji ingekuja; wangekufa kwa njaa mwaka uliofuata.

150 Ndugu, dada, mbegu inapandwa kwenye shamba lililolimwa na Roho Mtakatifu. Hebu na tuiache ishikilie, sasa, na ikue.

Yesu wa Nazareti, loo . . . [Ndugu mmoja ananena kwa lugha, ndugu mmoja anafasiri—Mh.]

151 Amina. Mumesikia jumbe hizo tatu? Biblia ilisema, “Kutakuwa na jumbe tatu kwa wakati mmoja.” Hizi hapa, na wa mwisho umewaendea wahubiri, mnaona, hizo zingine mbili kwa walei, huu nao kwa wahubiri. Ndugu, Mungu yuko miongoni mwetu; Mungu yuko miongoni mwetu. Hakika yuko. Na tumpe sifa.

152 Ee Yesu, Mwana wa Mungu, Mwana-Kondoo wa thamani, na ijulikane leo hii, Bwana, na ijulikane, Ee Mungu, tembelea Chicago kuliko hapo awali. Nyosha mkono Wako wa Mwanao mtakatifu, Yesu, kuwaponya wagonjwa na wanaoteseka. Fanya ishara na maajabu, Bwana, fanya mapito kusudi watu waweze kutembelea humo. Wabariki, Bwana. “Mpeni utukufu enyi watu wote, kwani Damu Yake inaweza kuosha kila doa.”

153 Jinsi tunavyokushukuru Wewe, Bwana. Jinsi tunavyotubu dhambi zetu. Jinsi tunavyokutazamia Wewe, Mwana-Kondoo wa Mungu, na kukuamini Wewe, ya kwamba Wewe ndiwe Mwana-Kondoo, Mtakatifu, wa pekee, Mungu wa kweli na aliye hai. Tunakupa sifa na utukufu, na—na kutubu, na kukuomba Wewe, Bwana, utusamehe. Na kutusaidia, Ee Mungu, tuwe vielelezo, si tu kuweka mipaka, katika haki pekee, na kuhubiri Neno wakati ufaao, na wakati usiofaa, kama ulivyotwambia tufanye.

154 Wabariki watu hawa, Bwana. Samehe kila dhambi. Utuondolee maovu yetu yote, na utuondolee mawaa yote; utuoshe kwa Damu Yako. Na jalia Mwana-Kondoo wa Mungu, loo, atufanye kila mmoja wetu kuwa kondoo, leo hii; utunyoe, Bwana, kutoka kwa majaliwa yetu ya kidunia ya mambo haya ya ulimwengu. Tuondolee mambo yote, na umjalie Hua wa Mungu akae juu ya kila moyo sasa hivi, ili kwamba huu utakuwa mojawapo wa nyakati kuu sana ambazo Chicago imewahi kuwa nazo. Ndivyo ilivyo, katika chumba hiki, alasiri ya leo, kwa sababu ya kuja kwa Bwana Yesu Kristo katika uweza Wake.

155 Ee Kristo, wapokee watu hawa, ninawaombea. Na wahudumu hawa, na mimi mwenyewe, tunaposimama hapa, Bwana, tukishuhudia, na tukijua ya kwamba Wewe uko katikati yetu, na tukijua ya kwamba tutasimama katika Uwepo Wako, siku moja, kutoa hesabu kwa ajili ya maneno yetu, hata kwa mawazo yetu. Nasi tunaomba, Baba, ya kwamba utatuosha na kutusafisha na dhambi zote. Na kutufanya kuwa na mioyo safi na nia safi, na kwa lengo moja: kuona watu wakizaliwa kwa Bwana Yesu Kristo. Utufanye tuwe na nia ya umishenari.

156 Ee Mungu, tujalie kuingia mitaani. Loo, sauti iko wapi mitaani? Hakuna mikutano ya mitaani tena. Hakuna chochote tena. Nao ulimwengu umekuwa mahali pamoja panaponuka, Bwana, loo, kwa sababu tumeachilia. Utusamehe, Bwana. Jalia tulie kama manabii wa kale. Loo, tusaidie, Mungu mpendwa. Tunaomba ya kwamba utapokea toba yetu, na kutuosha, na kutusafisha, na kutupa karama za Roho. Na uingie ndani yetu, Ee Bwana, upya leo hii, na tangu leo na kuendelea. Ninawasilisha maombi haya Kwako kwa ajili ya watu hawa na kwa ajili yangu mwenyewe katika Jina la Yesu Kristo.

157 Nini kimetokea? Hii ni nini? Jiulize swali hilo. Ni Roho Mtakatifu yeye yule ajuaye siri ya kila moyo. Na tupeane mikono sisi kwa sisi na kusema, “Ikiwa nimekudhuru au kufanya lolote, Mungu anisamehe.”

158 Hii ni kwenu, kwangu. . .kutoka kwangu kwenda kwenu: Ikiwa nimemkosea mtu yeyote, Mungu anisamehe. Kama nimeachilia au kupatana, Mungu anisamehe. Nataka kuwa mtumishi wa Bwana. Nataka kumpenda kila mtu. Na zaidi ya yote, nataka kumpenda Bwana, ili niweze kusimama kama m-. . .kati ya walio hai na waliokufa, kumtumikia. Nampenda. Natarajia jambo kuu kutokea sasa, tangu kuzuriwa huku kwa ajabu. Ninaamini hilo kwa moyo wangu wote.

> . . .nitamsifu,
> Msifuni Mwana-kondoo aliyechinjwa kwa ajili
> ya wenye dhambi;
> Mpeni utukufu enyi watu wote,
> Kwa maana Damu Yake inaweza kuosha kila
> doa. (Loo, jamani.)

Nitamsifu, nitamsifu,
Msifuni Mwana-kondoo aliyeyauawa kwa ajili
ya mwenye dhambi;
Mpeni utukufu enyi watu wote,
Kwa maana Damu Yake inaweza kuosha
madoa yote.

Nitamsifu, nitamsifu,
Msifuni Mwana-kondoo aliyechinjwa kwa ajili
ya mwenye dhambi;
Mpeni utukufu enyi watu wote,
Kwa maana Damu Yake inaweza kuosha kila
doa.

159 Tunapoinamisha vichwa vyetu katika ibada ya unyenyekevu, huku Ndugu Mattsson, ukituachilia tufumukane kwa maombi tafadhali, au maneno unayotaka kusema, ninapojitayarisha kwa ajili ya usiku wa leo.

56-1002A Baba, Saa Imekwisha Kufika
Philadelphia Church
Chicago, Illinois Marekani

SWAHILI

©2022 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

## Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:



Voice Of God Recordings

P.O. Box 950, Jeffersonville, Indiana 47131 U.S.A.

www.branham.org